# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA HANANG'**

## TANGAZO LA UKODISHAJI WA SHAMBA

Mkurugenzi Mtendaji (W) Hanang' anawatangazia wananchi wote, vikundi na taasisi kuomba mashamba ya Halmashauri yaliyopo eneo la Gawal lenye ukubwa wa ekari mia Sita na Kumi na Nne **(614)** na Bassotu lenye ukubwa wa ekari elfu nane mia Tano na Hamsini na Nne **(8,554)**. Mashamba yote mawili (2) yamepangwa katika Blocks/Vitalu na udongo umefanyiwa vipimo vya Afya ya Udongo na kutambua mazao ya kipaumbele katika kila kitalu/Block. Mashamba yote yana udongo wenye rutuba na kwamba katika msimu wa kilimo 2025/2026 ukodishaji utakuwa ni **TZs 250,000.00** kwa ekari kwa shamba la **GAWAL** katika **Vitalu vyote** ; na **TZs 100,000.00; TZs 150,000** na **TZs 200,000.00** kwa ekari kwa shamba la "**BASSOTU PLANTATION**" kulingana na **Kitalu** atakachopenda mwombaji.

### MASHARTI YA MAOMBI YA SHAMBA

1. Kila Mwombaji wa shamba aombe mwenyewe na anatakiwa kulipa ada ya maombi ya shamba kiasi cha Tshs **50,000.00** benki ya NMB au CRDB baada ya kupewa Bill (Control Number) kutoka ofisi ya **Mweka Hazina (W)** ambayo haitarudishwa.
2. Mwombaji ataje idadi ya ekari anazoomba kwa **Block /kitalu husika** kwenye shamba husika kati ya shamba la Gawal na Shamba la Bassotu.
3. Fomu hizo zinapatikana Ofisi ya Kitengo cha Usimamizi wa Ununuzi kuanzia leo tarehe **10/09/2025** hadi tarehe **19/09/2025** Halmashauri ya Wilaya ya Hanang'.
4. Fomu hii ijazwe kikamilifu na mwombaji na kupitishwa na Mtendaji wa Kijiji au Kata wa eneo analotoka/analoishi.
5. Mwombaji wa shamba ataingia Mkataba wa ukodishwaji kwa msimu moja tu baada ya kulipia ekari atakazopangiwa; Msimu ni **Oktoba,2025 hadi Septemba, 2026.**
6. Mwombaji wa shamba atatakiwa kulipa fedha zote za ukodishaji wa shamba ndani ya **siku kumi na nne (14)** baada ya kutangaziwa au kupatiwa taarifa ya Ekari alizopangiwa na ataingia mkataba na kupimiwa ekari alizolipia na kuoneshwa shamba ndani ya siku **saba (7) baada ya kulipia**.
7. Mwombaji wa shamba atatakiwa kulitumia shamba hilo kwa shughuli za kilimo cha mazao ya chakula na biashara (mazao ya msimu) tu.
8. Ikiwa Mwombaji wa shamba hatalima au hatavuna mazao kutokana sababu zozote zile, Halmashauri haitahusika na hasara hiyo.
9. Halmashauri haitahusika na hasara itakayojitokeza katika kulima shamba atakalokodishiwa na kwamba, gharama na majukumu yote yanahusu uendeshaji wa shamba atakalokodishiwa ni juu ya mkodishwaji wa shamba kwa kipindi chote cha mkataba.
10. Mkodishwaji wa shamba hatakiwi kuharibu makinga maji ambayo yapo katika shamba kwa kuyalima au kuyaondoa.
11. Kila mwombaji atakayefanikiwa kupata shamba, atapimiwa katika kitalu chenye kiwango sawa na malipo yaliyofanyika.
12. Hairuhusiwi mtu yeyote kulima shamba kabla ya kupewa au kugawiwa na Timu ya ugawaji ili kuepuka mazoea ya kutumia eneo lile lile.
13. Kamati itagawa shamba kwa mhusika aliyekodishiwa shamba na siyo mwakilishi kulingana na maombi ya Shamba.
14. **Mwisho wa kuleta maombi na kupokea maombi ya Shamba ni siku ya Ijumaa 19/09/2025 saa 9:30 alasiri katika Ofisi ya Manunuzi - Halmashauri ya Wilaya ya Hanang'.**



**Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya, Halmashauri ya Wilaya ya Hanang', 2 Barabara ya Amani,**
**S.L.P. 2, 27382 Ganana – Hanang', MANYARA. Simu Na. 027-2530022; Barua pepe:ded@hanangdc.go.tz;**
**Tovuti:www.hanangdc.go.tz**

NB: SIFA ZA UDONGO KATIKA VITALU NI KAMA ILIVYOAINISHWA HAPA:-

| BLOCK/ KITALU | Aina na Mazao ya Kipaummbele | Ekari | Ada ya Ukodishaji/Ekari |
|---|---|---|---|
| • Grade A (1&2);<br>• Murjanda-Gawal Rd ( 1-8);<br>• Njombe 7 (1-9 ) ;<br>• Makuyuni (1-4) Kambini - Bassotu Rd (1-4);<br>• Bassotu Rd (1-3) | **Mfinyanzi mweusi, mfinyanzi Mwekundu na kichanga (Tifutifu):** Dengu, Mahindi, Katam, Alizeti, Maharagwe. Ngano, Mbaazi, Girigilian. | 5123 | **200,000.00** |
| • Sekondari;<br>• Kambini - Murbadaw Rd (1-4);<br>• Uwanja wa ndege;<br>• Grade A (1&2);<br>• Murjanda-Gawal Rd ( 1-3);<br>• Njombe 7 (1-9 );<br>• Makuyuni (1-4);<br>• Kambini - Bassotu Rd (1-4);<br>• Bassotu Rd (1-3); | **Mchanganyiko wa Mfinyanzi mweusi na mwekundu na kichanga:** Mahindi, Alizeti, Maharagwe, Ngano, | 1,484 | **150,000.00** |
| • Kambini - Murbadaw Rd (1-4)<br>• Uwanja wa ndege; 373<br>• Murjanda-Gawal Rd (1-3); 365<br>• Njombe 7 (1-9 ); | **Mfinyanzi mwekundu na kichanga**: Mahindi, Alizeti, Maharagwe, Ngano, | 1,823 | **100,000.00** |
| Kona ya Murjanda (1 | Kichanga laini | 123 | Litatolewa Bure kwa atakayeliomba |
| **Jumla BASSOTU** | | **8,553** | |
| | | | |
| **Kitalu (A-H) - GAWAL** | Mfinyanzi mweusi, mfinyanzi Mwekundu na kichanga (Tifutifu): Dengu, Mahindi, Katam, Alizeti, Maharagwe. Ngano, Mbaazi, Girigilian. | **614** | **250,000.00** |

**Fomu zote za maombi zijazwe kwa ukamilifu na zirejeshwe katika ofisi husika:**

**Teresia A. Irafay**
**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA HANANG'**

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA HANANG

**NAKALA:**

1. Ofisi ya Katibu Tawala, S.L.P 10. **KATESH/HANANG'** - Wilaya ya Hanang
2. Watendaji wa Kata - Wajulisheni wakulima katika Kata zenu.
3. Mbao zote za Matangazo



**Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya, Halmashauri ya Wilaya ya Hanang', 2 Barabara ya Amani,**
**S.L.P. 2, 27382 Ganana – Hanang', MANYARA. Simu Na. 027-2530022; Barua pepe:ded@hanangdc.go.tz;**
**Tovuti:www.hanangdc.go.tz**